# HALI YA UISLAMU

# Maelezo ya kumsaidia Mkristo aufahamu Uislamu

Kosni nondiki mondo otigo e Yala Theological Centre, PO Box 765, Yala, Kenya, kod Siaya Theological Centre, PO Box 635, Siaya. Jandiko en Jim Harries (Jacob Otieno).

Hii kosi imeandikwa ili itumiwe kwa Yala Theological Centre, SLP 765, Yala, Kenya na Siaya Theological Centre, SLP 635, Siaya. Imeandikwa na Jim Harries (Jacob Otieno).

This course written by Jim Harries is for use at Yala and Siaya Theological Centres.

**2007**

Kaka itiyogo: japuonj idwaro mondo oelone jopounjore weche mantie mondi. Eka openjogi penjo mag gombaka. Eka penj man gi yiero adek en mar pimo winjo mar japuonjore.

Jinsi ya kuitumia: Mwalimu anatakikana awaeleze wanafunzi maneno ambayo yapo kwanza. Halafu maswali mengine yapo ya kuleta na kuhimiza mijadala.Swali linalokuwa na majibu tatu ni mtihani wa kuwauliza kwa wanafunzi mwishowe.

## Inayokuwepo

A. HISTORIA NA MSINGI WA UISLAMU
/1/ Utangulizi
/2/ Asili ya Uislamu – 1
/3/ Asili ya Uislamu – 2
/4/ Misingi ya Imani ya Uislamu

B. NGUZO (PILLARS) ZA UISLAMU, NA WANAWAKE KWENYE UISLAMU
/5/ Nguzo za *Shahada* (shuhuda) na Sala
/6/ Kufunga na Zaka
/7/ *Hajj*
/8/ *Jihad*
/9/ Wanawake ndani ya Uislamu

C. MIGAWANYIKO YA UISLAMU
/10/ Suni / Shia
/11/ Sufi
/12/ Islam wa Ahmadiya
/13/ Injili ya Barnabas

D. HADITH NA SHERIA
/14/ *Hadith* I
/15/ *Hadith* II
/16/ Sheria

D. KUWASAIDIA WAISLAMU
/17/ Uislamu wenye Mtego
/18/ Utetezi
/19/ Ukweli wa Mwungano wa Umungu na Uanadamu kwa Kristo
/20/ Umoja na Nafsi Tatu za Mungu

## A. HISTORIA NA MSINGI

**/1/ Utangulizi** Ibrahimu alimwamini Mungu. Kuamini Mungu mmoja kwake kulimfanya ahamie nchi ya Kanani, mahali ambapo siku hizi panaitwa Israeli. Mjukuu wake mmoja Yakobo alizaa Yuda. Wazao wa Yuda mpaka sasa wanaitwa Wayahudi, na wanafuata imani ya Kiyahudi.

Yesu Kristo alikuwa Myahudi. Jina lake linamaanisha 'Mungu anaokoa, aliyepakwa'. Alitumwa na Mungu, na yeye alikuwa Mungu. Alikuja duniani ili afe kwa ajili ya dhambi ya watu wote, ili yeyote amwaminiye apate kuokoka. Baada ya muda imani ya Ukristo na Uyahudi uligawanyika. Mpaka sasa Wayahudi wengi hawajamtambua Yesu kuwa Mwokozi.

Karne sita baada ya kuzaliwa kwa Yesu, kanisa lake lilikuwa limeenea sana. Wakati ule matawi ya kanisa yalikuwa yanajadiliana sana kufahamishiane juu ya hali ya Kristo -

aliyekuwa binadamu halisi na pia Mungu halisi kwa mwili mmoja. Umuhimu wa ukubaliano huo ulizusha ugomvi mwingi, mpaka ukatili na vita vikatokea.

Muhammad alipozaliwa wakati ule, alisikia hayo maneno ya ubishi kati ya Wakristo. Inaonekana alikuwa mtu aliyependa mambo ya Mungu. Kumwoa mjane tajiri kulimpa mali na muda wa kutosha kutafakari juu ya dini. Alipata maono, ambayo alisema yalitoka kwa malaika Jibrail. Maono yake yalijaribu kumaliza ugomvi uliokuwepo kati ya Wakristo kwa kusema: Yesu sio Mungu, na hata hakufa. Dini ya Uislamu iliweza kusambaa kwa urahisi kupitia vita dhidi ya nchi ya Wakristo waliokuwa wadhaifu sababu ya ugomvi wao.

1. Wayahudi wanaitwa hilo jina kulingana na nani mtu wa zamani wao? Babu wake alikuwa nani mwenye imani thabiti kwa Mungu?
2. Kulingana na ujuzi wako kiBiblia – nini ilifanya Wakristo na Wayahudi wagawanywe njia?
3. Muhammad alijaribu vipi kusuluhisha ugomvi ulivyokuwa kati ya Wakristo?
4. Kati ya dini ya Uyahudi, Ukristo na Uislamu gani ilikuwa iliotangulia, iliokuwa ya pili, na iliotokea nyuma? Fafanua.
5. Unaonaje hali ya kuendeleza dini kupitia vita?
6. Swali lingine?

Muhammad alidhania ni nani aliyempa maono?

A. Yesu
B. Musa
C. Jibrail

**/2/ Asili ya Uislamu – 1** Muhammad alizaliwa Mekka – mji uliokuwa tayari wakati ule penye *hajji* (pilgrimage) wa watu waliokuja kukiona 'kaaba'. Kaaba iko na jiwe jeusi, inasemekana lilitoka mbinguni, na hapo Waarabu walikuwa wanaomba miungu mingi kuanzia zamani – (inasemekana Miungu ilikuwepo 360). Wayahudi na Wakristo pia wakati ule walikuwa wanaishi Arabia. Inaonekana Muhammad alijifunza mambo ya Biblia na Ukristo kwa hawa.

Kulingana na Waislamu, Muhammad alizaliwa miaka 570 baada ya kuzaliwa kwa Yesu. Alikuwa mtoto yatima, kwa hivyo alilewa na baba mdogo. Alikuwa mfanye biashara mpaka alipomwoa Khadija (mjane mwenye mali). Kuoa penye mali kulimwezesha Muhammad kuanza kushugulikia maswali ya dini. Khadijah alimzalia watoto saba, lakini kati ya hawa sita waliaga kabla ya kufika umri wa kuzaa. Fatimah peke aliendelea kuzaa wavulana wawili Hassan na Hussain. Baada ya kifo cha Khadija Muhammad aliwaoa wake wengine kumi na wawili.

1/ Eleza hali ya 'kaaba' a. Awali. b. Sasa.
2/ Mtoto gani wa Muhammad aliishi na kukomaa?
3/ Jinsi Muhammad alilelewa na kuoa linatufundisha nini juu yake?
4/ Tunaonaje Muhammad kuoa wanawake 13?
5 Swali lingine?

Mke wa kwanza wa Muhammad alikuwa:

A. Myahudi
B. Mjane
C. Maskini

**/3/ Asili ya Uislamu 2** Waliosilimu (ingia kwa Waislamu) wa kwanza kulingana na mahubiri ya Muhammad walikuwa wenye jamaa yake na watu wa karibu. Raia wa Mekka walijaribu kuwaangamiza Waislamu wachache waliokuwepo wakati ule. Walisema Muhammad amepagawa. Mwaka 622 BK Muhammad alikimbia na wafuasi wake mpaka Medinah. Kukimbia kwao kiliitwa *hijrah*. Watu wa Medina walikuwa wakimwalika Muhammad ili awe kiongozi wa mji wao. (Wakati ule hata Wakristo na Wayahudi wengine walifurahiwa na Muhammad kabla upingamizi wake kali kwao haujadhihirishwa.)

Baada ya miaka chache Muhammad alishinda wa Mekka na vita. Kuanzia hapo vita vya kusambaza dini ilikubaliwa na Waislamu. Mwanzoni Muhammad aliiona Uislamu ikiwa dhehebu ya Wayahudi, lakini sababu Wayahudi hawakumkubalia alibadilika aiweke dini ya kipekee. Wakati ule aliwacha kusema waombe wakielekea Yerusalemu, na aliamrisha maombi yawe wa watu wakielekea Mekka. Alipokuwa Medinah aliweka misingi mingi ya dini - kwa mfano kuweka ijumaa siku ya kuomba, na Ramadan mwezi wa kufunga. Vita vikaendelea mpaka Waarabu wote walikuwa chini ya Uislamu.

632 Muhammad alikufa. Abu Baker aliwaongoza Waislamu kwa miaka miwili. Caliph Umar aliongoza 634 – 644, halafu Caliph Uthman. Uislamu ulienea sana kupitia vita. Wasingalishindwa kwa vita France 732 BK pengine wangalichukua hata Ulaya. Kwa kiasi kikubwa sana, kanisa lililokuwa Afrika kaskazini lilishindwa na Waislamu.

1/ Kwa nini raia wa Mekka mwanzoni hawakufurahia mafundisho ya Muhammad?
2/ *Hijrah* ni nini?
3/ Kwa nini Muhammad alibadilisha sheria ili watu waombe wakielekea Mekka badaala ya Yerusalemu? Jadili.
4/ Iliweza kuwa nini iliwasaidia Waislamu kuenea sana kwa miaka michache?
5/ Swali lingine?

Muhammad aliaga:
A. AD. 632
B. AD. 622
C. AD. 732

**/4/ Misingi ya Imani ya Uislamu** Misingi iliopo ni sita:
1. Mungu (Allah) ni mmoja tu. Kusema anao wenzake ni dhambi mbaya kwa Waislamu, inayoitwa *Shirk. (la ilah illa Allehu – hakuna Mungu mwingine ila Allah)*
2. Malaika waliumbwa na Allah ili wamsaidia kuwaangalia na kuwatunza binadamu. Kwa mfano Jibrail (anayeitwa pia *Rul ul'Amin* au Roho Mtakatifu), Mikaili, Israfili na Izraili. Malaika waliumbwa kutoka kwa nuru, lakini Jinn kutoka kwa moto. Jinn ni kama mapepo. Satani (au *ibilis*) pia yuko.
3. Vitabu vitakatifu vilikuwa 104, lakini vinabaki tu vinne. *Taurah, Zabur*, *Injil* na Qur'an (Korani). Sababu Wayahudi na Wakristo waliharibu vitabu vyao, Waislamu wanasema, Allah alikituma Qur'an kuwa kitabu cha mwisho.
4. Nabi. Waislamu wanatambua watakatifu wengi wa Biblia, k.m. Abrahamu, Daudi, Musa, Yesu, kama manabi. Nabi wa mwisho wanasema ni Muhammad. Waislamu hawaabudu manabii, ila Mungu (Allah).
5. Siku za hukumu na ufufuo inafafanuliwa sana kwenye Qur'an. Waislamu wanaaminiYesu atakuja siku ya mwisho – akiwa Mwislamu kuokoa Waislamu. Vitendo vya watu vitapimwa. Wenye dhambi wataanguka kwenye moto wakipitia daraja fulani (*sirat*) nyembamba.

*6. Taqdir* inamaanisha Allah anauwezo wote! Allah ameshaamua juu ya maisha ya kila mtu, mwisho wa mtu umeshaamuliwa naye, kwa hivyo jukumu la mwamini ni kumkubalia Allah kwa unyenyekevu wote.

Q. (Qur'an) 39:68 "Na litapigwa barugumu watoke roho watu waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule amtakaye Mwenyezi Mungu. Tena litapigwa mara nyingine. Hapo watafufuka (wote); wawe wanatazama (nini litatokea)."

Q. 23:102-103 "Ama wale ambao mizani ya amali zao (nzuri) itakuwa nzito, hao ndio wenye kufaulu. Na wale ambao mizani yao itakuwa nyepesi, hao ndio waliozitia hasarani nafsi zao, na katika Jahanamu watakaa muda milele."

9. Q.16:97 Wafanyaji mema, wanaume au wanawake, hali ya kuwa ni Waislamu, tutawahuisha maisha mema, na tutawapa ujira wao (Akhera) mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokuwa wakiyatenda.

1/ Jadili juu ya *shirk*.
2/ Je, Waislamu wanaviamini vitabu vya Wakristo? Kwa nini?
3/ Eleza 'siku ya mwisho' ya dunia, kulingana na Waislamu.
4/ Jadiliana juu ya ufahamu wa Uislamu kusema Mungu ameshaamua kila kitu, na jukumu la mwamini ni kumkubalia tu.
5/ Swali lingine?

Kulingana na Waislamu, Yesu alikuwa:

A. Nabi
B. Aliyepakwa
C. Mwokozi

## B. NGUZO (PILLARS) ZA UISLAMU, NA WANAWAKE KWENYE UISLAMU

**/5/ Nguzo za *Shahada* (shuhuda) na Sala** Shuhuda ni ya imani ya Mwislamu na inatajwa mara nyingi. Inatolewa kwa Qur'an, sura ya kwanza.

Muislamu lazima ajitawaze kabla hajaomba. *Wudu* ni kusafisha uso, mikono, tena kichwa, halafu miguu na maji. Sheria nyingi ndogo ndogo pia inahusika na kutawadha vile inayofaa – k.m. jina la Allah litajwe, maji yawekwe umani mara tatu, kuchanua ndevu na vidole vyenye maji, n.k.. Mwislamu anafundishwa asipotawadha vizuri, maombi yake yanaweza kuwa bure. *Ghusl* ni kujisafisha na maji kujitakasa baada ya kuwa najisi. *Tayammum* ni kutumia mchanga au udongo kujitawadha ikiwa maji hayapo.

Mtu anaweza fanya sala popote, lakini akielekea Mekka, na sala bora yanakuwa Msikitini. *Adhan* ni mwito kwa maombi ambayo inatangazwa kutoka msikiti juu na *muezzin*. Wakati wa maombi sehemu za Qur'an zinasomwa. Waombaji wanainama chini. Kipindi kimoja cha maombi kinaitwa *rakaat*, na inaweza rudiwa mara kadhaa. Maombi yanatakikana mara tano kwa siku. Ijumaa mchana Imam anatoa hotuba kabla ya maombi. *Dua* ni aina ya maombi tofauti inayofanywa kwa hiari.

1/ Eleza sehemu muhimu za shuhuda.
2/ Kwa nini kutawadha? Fafanua.
3/ Jadiliana juu ya vile Waislamu wanavyofanya sala zao.
4/ Fafanua utofauti kati ya sala za Waislamu na za Wakristo
5/ Swali lingine?

Waislamu wanatakikana wasali mara ngapi kila siku? A. 10
B. 3
C. 5

**/6/ Kufunga na Zaka** Kufunga ni kutokula wakati wa mchana, lakini Waislamu hukula usiku. Kufunga ni lazima kwa mwezi wa *Ramadan* (ila kwa wamama wajawazito, wanaonyonyesha, wakongwe, watoto, wanaougua n.k.). Mara nyingi uwezo wa kazi unalegea wakati wa Ramadan. *Id-ul-fitre* ni siku ya kusherekea mwisho wake. Mtu asipofuata sheria zote za kufunga anaweza lazimishwa kulipa, kwa mfano kwa kuendelea kufunga baada ya Ramadan kuisha.

Zaka ni lazima. Sadaka inatolewa kwa hiari mwisho wa Ramadan. Waislamu wote waliokomaa wanatakikana watoe zaka ya asilimia 2.5 kwa mali yao yote kila mwaka. Zaka inaweza tolewa kwa maskini, wasafiri, waliosilimu (badilisha kuwa Waislamu) karibuni n.k. Inaweza tumiwa kwa *jihad* lakini kwa hakika haitakikani itumiwe kujenga msikiti au kumsaidia mwenye jamaa wa karibu.

1/ Eleza sheria za Ramadan.
2/ Eleza kwa mawazo yako – kufunga Ramadan ina uzuri gani na ubaya gani?
3/ Asilimia gani inatolewa zaka, na akina nani wanapewa? Jadiliana.
4/ Eleza utofauti kati ya zaka/sadaka za Ukristo na Uislamu.
5/ Swali lingine.

Mtu anatakikana atoe asilimia gani ya mali yake kwa zaka kila mwaka:

A. 10
B. 2.5
C. 5

**/7/ *Hajj*** *Hajj* (kusafiri mpaka Mekka mwezi wa *Dhul Hijjah*) ni lazima kwa Waislamu wenye uwezo (wenye chakula kutosha na pesa za usafiri) kulingana na Q 22 : 27 – 29 na Q 3 : 97. *Hajj* inakuwa ukumbusho hata kwa Abrahamu ambaye, kulingana na Waislamu, alikuwa hapo Mekka.

Q. 22:27-29 "Na (tukamwambia) "Utangaze kwa watu habari za *Hija*, watakujia, (wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyekonda (kwa machofu ya njiani wakija kutoka katika kila njia ya mbali; Ili washuhudie manufaa yao na (ili wakithirishe) kuitaja jina la Mwenyezi Mungu – katika siku zinazojulikana (fadhili zake) – juu ya yale aliyowaruzuku, nao ni wanyama wenye miguu minne. Na kuleni katika wanyama hao na mlisheni mwenye shida aliye fakiri. Kisha wajisafishe taka zao, na watimize nadhiri zao, na waizunguke nyumba ya Kale, (nyumba kongwe – *Al-Kaaba*)"

Q.3:97 "Humo mna Ishara zilizo wazi (za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake. Miongoni mwa hizo ni) mahali alipo kuwa akisimama Ibrahimu, na anayeingia (nchi hiyo) anakuwa katika salama. Na mwenyezi Mungu amewawajibishia watu wafanye Hija katika Nyumba hiyo; yule awezaye kufunga safari kwenda huko. Na atakaye kanusha (asiende, na hali ya kuwa anaweza) basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kuwahitajia walimwengu."

Wakishafika 'kaaba' wasafiri wanavaa mavazi meupe na kuizungusha jiwe jeusi mara saba. Msafiri anatakikana alibusu jiwe, linalosemekana lilitoka mbinguni. Sala fulani inatajwa wakati ule. Nguzo tatu zinapigwa na mawe. Baadaye msafiri ataitwa jina la heshima *hajj* au *hadji*. Karibu mambo hayo yote yanayofanywa Mekka ni hayo hayo yaliofanywa na Waarabu wapagani kabla ya kuanzishwa kwa Uislamu.

1/ Inatakikana akina nani aende kwa hajj?
2/ Watu hufanyaje pale Mekka kwa hajj?

3/ Eleza hali ya jiwe jeusi.
4/ Kwa nini hivi vitendo vya Waarabu wapagani kabla ya wakati wa Uislamu vinaendelea kufanywa na Waislamu?
5/ Swali lingine?

Wakina nani walikuwa wanasafiri kuenda Mekka kabla ya wakati wa Islamu:
A. Wakristo
B. Waarabu wapagani
C. Wafuasi wa Abrahamu.

**/8/ *Jihad*** Wengine husema *jihad* ni nguzo ya sita ya Uislamu. Imejadilianiwa sana na watu wanaojiuliza ikiwa ni haki kwa Mwislamu kueneza dini na nguvu.

Q. 2:256 Inasema "Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini …" Lakini tukisoma Q. 9:5 tunakuta maneno hayo: "… basi waueni (piganeni na) washirikina [watu ambao sio Waislamu] popote muwakutapo, na wakamateni mateka (kama wanavyokufanyeni) na wazungukeni na wakalieni katika kila njia." Wasomi Waislamu wanatuambia ikiwa sehemu mbili za Qur'an zisizokubaliana, ile iliokuwa ya baadaye inaaminika. Sababu sura ya tisa iliandikwa baada ya sura ya pili, sura ya tisa ina chakuliwa sawa – kwa hivyo kuwalazimisha watu wawe Waislamu kunaruhusiwa.

*Hadith* inasisitiza umuhimu wa vita ili dini iendelezwe. Vita hivyo vinaitwa *Jihad*, na vinafanya watu wengi wauwawe Nigeria na Sudan siku hizi. Pia iko *jihad* ya ushuru – wasio Waislamu penye utawala wa Islamu wanalipishwa ushuru unaoitwa *Al-Jizya*. Iko *jihad* ya kulipa pesa kwa wale wanaogeuka ili wawe Waislamu. Kufuatana na sheria ya Uislamu, atakayewacha Uislamu atauawa. Mwislamu anayekufa akiwa anapiga vita vya jihad, ataenda mara moja Paradiso.

1/ Kwa nini Q. 2:256 inasema tofauti na Q. 9:5? Tuamini nini? Kwa nini?
2/ Je, Mwislamu anaruhusiwa kumwua Mkristo?
3/ *Al-Jizya* ni nini?
4/ Jinsi gani nyingine Waislamu wanajaribu kufanya watu waingie dini yao?
5/ Swali lingine?

*Al-Jizya* ni nini?
A. kifo
B. vita
C. ushuru

**/9/ Wanawake ndani ya Uislamu** Waislamu wanaweka wanawake ndani ya nyumba, na kushugulikia kazi za nyumba. Waislamu wanaamini mwanamke lazima ajifunike mwili wake vizuri – asipofanya hivyo anawaweka wanaume kwa majaribio yatakayowashinda. Waislamu wote wanatakikana waoe. Mwanamume Mwislamu anaruhusiwa kuwaoa wanawake Wakristo au Wayahudi, lakini msichana Mwislamu lazima aolewe tu na Mwislamu.

Mwislamu anaruhusiwa kuwaoa wanawake wanne. Ni rahisi kwa mwanaume kumfukuza mwanamke, lakini sio rahisi mwanamke kumkimbilia mumewe. Washia (dhehebu ya Uislamu) wanaruhusiwa kufanya 'ndoa ya muda', k.m. sali moja tu, au miaka kadhaa. Upangaji wa jamii unaruhusiwa, lakini sio utoaji wa mimba. Watoto wote wa baba Mwislamu ni Waislamu. Q. 16:47 inasema mbingu ni sawa kwa wanawake na wanaume. Lakini mbinguni wanaume wanatumikiwa na wasichana warembo, na Qur'an haisemi wanawake pia wanakuwa na watumishi wao kwa mbingu yao. Kwa njia nyingi Uislamu

unaegemea pande ya mwanaume. Kwa Sheriah, mwanamke anakuwa na nusu ya dhamani ya mwanaume.

1/ Tunaonaje hali ya wanawake kujifunika mwili wao?
2/ Tunaonaje hali ya maongezeko ya Waislamu kwa njia ya kuzaa?
3/ Eleza ubaya na uzuri kwa hali ya mwanamke kwa Islamu.
4/ Inatakikana mwanamke awe na dhamani gani kando ya mwanaume?
5/ Swali lingine?

Mwislamu anaruhusiwa kuoa wanawake wangapi?

A. 4
B. 1
C. 6

## C. MIGAWANYIKO YA UISLAMU

**/10/ Suni / Shia** Wengi Waislamu ni Wasuni. Kwa dunia ni asilimia 90. Sehemu mbali mbali Wasuni wanawadhulumu Washia. Uislamu unaojulikana zaidi kwa Afrika Mashariki ni suni. Watu weusi duniani wengi wao wako kwa Suni. Mfano wa Shia Afrika Mashariki ni Waishmael, (kwa jina lingine Aga Khan).

Shia iligawanywa mapema sana. Baada ya Abu Bakar, Umar na Uthman, Ali alikuwa kiongozi wa Waislamu. Alikuwa mumewe msichana wa Muhammad aliyeitwa Fatima. Wakati wa Ali ugomvi ulikuwa kali juu ya uongozi wa Waislamu. Baada ya kuuawa kwa Ali watoto wake Hussain na Hassan waliendelea kushindana kupata uongozi mpaka hawa pia wakauwawa. Wanaoamini Ali alikuwa kiongozi halisi wa Uislamu wanaitwa Washia.

Washia wanapenda kusherekea kifo cha Hussain. Wanaamini wajukuu wa Ali peke kuwa Waimam ya kweli, na wanaamini hawana kosa au dhambi zozote. Washia wanaweza kutafsiri au tafakari Qur'an, baadala ya kuiamini tu vile Wasuni wanavyofanya. Washia wamegawana sana kwa dini ndogo nyingi. Washia wanaruhusiwa kusema uongo, ikiwa bado wanaamini ukweli ( kufanya hivyo wanaita *taqiya*). (Kwa kiasi hata Wasuni pia wanaruhusiwa kutaja uongo.)

1/ Kwa nini Waafrika wengi ni Wasuni, sio Washia?
2/ Eleza sababu unaona Washia wanawaamini sana watu wa Ali? Kulingana na wewe – nani ni sawa (au bora)?
3/ Eleza utofauti umeshaona kati ya Suni na Aga Khan (Waishmael)?
4/ Unaonaje hali ya dini inayoruhusu uongo?
5/ Swali lingine?

Mumewe Fatima (msichana wa Muhammad) aliitwa nani?

A. Ali
B. Abu Baker
C. Hussain

**/11/ Sufi** Hawa ni wa 'roho' ndani ya Uislamu! Jina limetokea kwa hali ya mmoja wao aliyevaa nguo ya sufu. Waanzalishi wa hiyo dhehebu ndani ya Uislamu, walipenda maisha safi sana, utaratibu, na kujitolea kwenye kelele za maisha duniani. Wanapenda kutengeneza uhusiano na Mungu kiroho kwa njia mbali mbali, kwa mfano kwa kutaja na kurudia rudia kulitaja jina la 'Mungu' mara nyingi.

Wasufi wanaweza kuwa ndani ya dhehebu mbali mbali ya Uislamu. Waislamu wengi hawawapendi. Sababu ni badala ya kukaza hali ya kufuata sheriah, wanataka *kumfahamu* Mungu. Vitendo vyao vingine ni kama wamejifunza na Wakristo. Wasufi wanaweza kulegea kwa sheriah za Uislamu mbali mbali. Kwa mfano, wanaume na wanawake wanaweza omba mahali pamoja. Wasufi wamekuwa wamisionari wa Waislamu. Maendeleo yao kwenye upendo na kumfahamu Mungu yanawafanya wawe karibu kwa Ukristo.

1/ Ni vipi wengine husema Wasufi wako karibu na Wakristo?
2/ Kwa nini Waislamu wengi hawawezi kufurahia vitendo vya Wasufi?
3/ Wasufi wanaofuata upendo na Roho – je, wanaingia kwa dini ya Ukristo, au ni Waislamu tu waliopotea?
4/ Je ni kweli Waislamu wanakaza sheria kushinda Wakristo? Vipi?
5/ Swali lingine?

Wa 'roho' wenye Waislamu wanaitwa:
A. Waroho
B. Wasufi
C. Waupendo.

**/12/ Islam wa Ahmadiya** Dini hii ilianzishwa na Mhindi aliyeitwa Mirza Ghulam Ahmad Qadiani mwaka wa 1889. Alisema yeye mwenyewe ni Messiah. Ahmadiya sasa imeenea kwa inchi nyingi, pamoja na Kenya. Waahmadiya wanafuata imani nyingi kama Waislamu wengine, kwa mfano wanafunga wakati wa Ramadan, na wanaomba mara tano kila siku. Lakini wanatofautiana kwa mambo mengine, ambayo imefanya Waislamu wengine kusema Waahmadiya sio Waislamu halisi.

Kwa mfano, wanasema Muhammad hakuwa nabi wa mwisho, ila nabi mkuu, na manabi wengine bado wanaweza kujitokeza. Pia, tofauti na Waislamu wengine ambao wanasema Yesu hakusulubishwa, na Wakristo ambao wanasema alikufa msalabani, Waahmadiya wanasema Yesu hakufa msalabani ila alizirai tu, halafu baada ya kupona alienda India na akawahubiria kabila kumi ya Israel waliofukuzwa na Nebukadnezar. Baadaye Yesu, wanasema, aliaga tu. Kwa hivyo kulingana nao Yesu hatarudi kumaliza Ukristo vile Waislamu wengine wanaoamini, lakini Ukristo utaishiwa kulingana na kushindwa kwa Wakristo kwa mijadala.

1. Kwa nini Waislamu wenzao wanasema Waahmadiya sio Waislamu?
2. Kwa nini, unafikiri, Waahmadiya wanasema Muhammad hakuwa nabi wa mwisho?
3. Eleza utofauti ya Ahmadiya na Waislamu wengine kwa panda ya imani yao juu ya kurudi kwa Yesu.
4. Ni vipi ugawanyiko wa Waislamu na Wakristo unafanana, na unatofautiana?
5. Swali lingine?

Kulingana na Waahmadiya, Yesu:
A. Alizirai tu msalabani.
B. Alikufa msalabani
C. Hakusulubishwa

**/13/ Injili ya Barnabas** Waislamu wanataja 'Injili ya Barnaba' kujaribu kuchanganya Wakristo. Wengine husema injii ya Barnaba ni ya asili ya kwanza, na Agano Jipya ilikuja baadaye. Hii injili inasema Barnaba alikuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu, na inamweleza Yesu kama mtengenezaji wa njia kwa huyu anayetajwa kuwa Muhammad.

Mwandishi wa hii injili anakataa mafundisho ya Paulo – ambayo ni ngumu kuamini sababu Barnabas na Paulo walikuwa watu wa karibu sana. Inasema Muhammad ni *messiah*, jambo ambalo Qur'an yenyewe inakataa. Utafiti umedhihirisha kwamba Injili ya Barnaba iliandikwa miaka 1400 au zaidi baada ya kuzaliwa kwa Yesu! Makosa yaliyopo yana dhihirisha hayawezi kuwa yaliandikwa awali wakati wa Agano Jipya.

1/ Inaonekana Injili ya Barnaba iliandikwa lini?
2/ Injili ya Barnaba inaeleza Yesus kama nani?
3/ Kwa nini Barnaba wa Agano Jipya hawezi kuwa ameandika hii Injili?
4/ Kwa nini injili ya Barnaba iliandikwa?
5/ Swali lingine?

Injili bandia iliyoandikwa miaka zaidi ya 1400 baada ya Kristo inaitwa:

A. Injili ya Barnaba
B. Injili ya Jonas
C. Injili ya Luka

## D. HADITH NA SHERIA

**/14/ *Hadith* I** Waislamu wanayaamini maandiko mengine matakatifu yanayoitwa *Hadith* pamoja na Qur'an. *Hadith* inaeleza juu ya maisha na maneno ya Muhammad ambayo hayapo kwenye Qur'an. Tutachunguza kidogo *hadith* ambayo Al-Bukhari alisanya – *hadith* 7,275 ambayo hakukuwana shaka juu yao. (Aliwacha nje *hadith* ingine nyingi sababu hakuamini kabisa ilikuwa sawa.)

*Hadith* inatueleza jinsi, kabla ya kugeushwa kwa Waislamu, Kaaba ilikuwa na sanamu 360. Kwa hivyo inaeleza mambo mengi juu ya Uislamu na historia yake. Kwa sehemu kubwa *Hadith* inaeleza mambo mengi juu ya maisha ya Muhammad, ambayo Waislamu wanajaribu kuiga ili waingie mbinguni.

*Hadith* inasisitiza Muhammad alikuwa mtu mweupe. Watu weusi wote wanaotajwa ni watumwa – na hata Muhammad alikuwa na mtumwa mweusi (*Hadith* 6/435). Kulingana na *Hadith* Muhammad alikuwa mwepesi kwa hasira. Kulingana na *Hadith*, Muhammad alikuwa mwenye dhambi, sababu aliende kuomba samaha kwa Mungu mara nyingi (8/319). Pamoja na dhambi yake ilikuwa akikata mikono na miguu ya watu, kutoa macho yao na chuma, na kuwafanya watu wafe kwa kiu ya maji (*Hadith* 1/234, 8/796). Muhammad pia alikuwa na wake wengi, na wanawake wengine tena wengi ambao hawakuwa wake halisi. Qur'an inasema Muhammad hakufanya miujiza yo yote, lakini *Hadith* ina maelezo juu ya miujiza mingi ambayo Muhammad alifanya.

Kuongea vibaya juu ya Muhammad kunawaudhi Waislamu sana, sababu wanajaribu sana kuyaiga maisha yake.

1/ *Hadith* ni nini?
2/ Kwa nini Waislamu wanayaiga maisha ya Muhammad?
3/ *Hadith* inaonyesha kwa njia nyingi maisha ya Muhammad hayakuwa vizuri. Sasa inawabidi Waislamu waige hata ubaya wake?
4/ Kwa nini kuongea mbaya juu ya Muhammad inawaudhi Waislamu sana?
5/ Swali lingine?

Mkusanyaji wa *Hadith* alikuwa:

A. Al-Bukhari

B. Muhammad
C. Abu Baker

**/15/ *Hadith* II** *Hadith* inaeleza – Qur'an haikusanywa mpaka baada ya kifo cha Muhammad. Ilisanywa na Uthman. Halafu Uthman akajaribu kushugulika ili maandiko mengine ya Qur'an yote yachomwe. Kwa hivyo awali Qur'an haikuwa moja tu. *Hadith* inasema (*Hadith* 6/509) sehemu ingine ya Qur'an haikuweza kuandikwa chini sababu waliofahamu peke yao walikufa bila kuandika.

*Hadith* inasema mtu hawezi toka kwa Uislamu. Inasema mtu akitoka, lazima auawe (9/64). *Hadith,* kama vile Qur'an, inasema Wayahudi na Wakristo wanaelekea moto wa Jehanamu. Muhammad aliona ni vibaya sana mtu kujichafua na kojo yake – kujichafua na kojo itamfanye mtu aingie Jehanamu. Sheria juu ya kukojoa zinasema mtu asikojoe akielekea Mekka, na asibebe sehemu yake na mkono wake wa kulia. Inasema Setani atakojoa masikioni mwa watu wanaolala wakati wa sala (2/245).

Kama Qur'an pia, *Hadith* inakubali sehemu fulani yake imepitwa na maneno ya baadaye, kwa hivyo inaondolewa. (Vile tulivyo jadiliana juu ya Qur'an juu, ikiwa vitu vinavyotajwa sehemu mbali mbali ya *Hadith* hazikubaliane, ya kwanza inaondolewa, maana yake haiaminiki.)

1/ Eleza jinsi maneno ya Qur'an yaliosanywa?
2/ Utasemaje kwa wale wanaosema Qur'an ni moja tu?
3/ Inakuwaje mtu akiacha Uislamu?
4/ Kwa nini *Hadith* inakuza umuhimu wa jinsi ya kukojoa?
5/ Swali lingine.

Kulingana na Hadith, anayekojoa asielekee wapi?
A. Mashiriki
B. Mekka
C. Nyumbani

**/16/ Sheria** Zinakuwepo sheria nyingi zinazojaribu kuongoza kila sehemu ya maisha ya Waislamu. Hapo Uislamu unakuwa mbali sana na Ukristo. Waislamu wanataka sheria itawale dunia nzima. Ikiwa hivyo, wasio Waislamu (wanaoitwa *dhimi*) wanaadhiriwa sana-kwa mfano kulipizwa ushuru.

Sheria zinatoka kwa Qur'an na pia *Hadith*. Halafu viongozi wa dini wanaweza endelea kuziunda sheria zingine. Wasuni wamegawiwa chini ya sheria aina nne: *Nanafi*, *Maliki*, *Shafii* na *Hanbali*. (Sheria ya Washia zina fanana sana na hizi.) Sheria zinakuwa kali, kwa mfano mkono wa mwizi unaweza katwa, na anayewacha dini anaweza uawa. Sheria ina dumaaza wanawake. Sheria ziliundwa kati ya 700 na 860 AD, na sasa haziwezi kubadilishwa tena, kwa hivyo zimepitwa sana na wakati. Waislamu ambao wanataka sheria zisiwe kali hivyo, wanayahatarisha maisha yao.

1/ Eleza utofauti unaona kati ya sheria kwa Wakristo na kwa Waislamu.
2/ Wa Sunni wanazo aina za sheria ngapi?
3/ Kwa nini Waislamu wasibadilishe sheria ili ifae kwa maisha ya siku hizi?
4/ Je, Wakristo wanatakikana wajitetea kwa Waislamu wanaotaka kuwaweka chini ya sheria zao?
5/ Swali lingine?

*Dhimi* ni watu aina gani?

A. Wa Saudi Arabia
B. Wasio Waislamu
C. Waislamu wanawake

**E. KUWASAIDIA WAISLAMU**

**/17/ Uislamu wenye Mtego** Uislamu ni dini inayopinga Ukristo. Wakati Wakristo wa dunia walikuwa wanagombana juu ya hali ya Mungu ndani ya Kristo, Waislamu waliposema Yesu sio mungu kabisa, walipotea mbali na ukweli. Maandiko takatifu ya Wakristo (Biblia) hailingane na imani ya Waislamu. Waislamu husema wanaamini *Torah*, *Zabur* na *Injil*, lakini ukweli ni hawaviamini vitabu ambavyo viko vinavyoitwa hivi. Wanaamini Wakristo na Wayahudi wameyachafua maandiko hayo. Yanayokuwepo yamechafuliwa na ya asili yamepotea kulingana na Waislamu. Huo uwongo ni moja wa misingi ya dini yao.

Uislamu ni dini ya chuki. Inafundisha kukuwa na uadui, na kulipa kisasi kwa huyu anayekukosea – mbali sana na mafundisho ya Kristo. Waislamu wanaweza kataa hivyo, sababu wanaruhusiwa kutaja uongo! Uislamu kama dini ni mtego. Kuingia ni rahisi (mtu akubalie tu Allah, na Muhammad nabii wake), lakini kutoka ni kifo. Aliyetoka Uislamu, Waislamu wengine wanaruhusiwa kumwua. Sababu Mwislamu anamwogopa sana Mwislamu mwenzake – Waislamu hawana uhuru kuongea ubaya yoyote juu ya dini yao. Badala yake wanalazimishwa kupiga kelele pamoja upingamizi wa dini yao unapotokea. Uislamu pia unajaribu kuzuia maendeleo mengi, sababu washirika wanalazimishwa kuzifuata sheria ambazo haziambatani na maendeleo.

1/ Waislamu wakisema wanaiamini *Torah*, *Zabur* na *Injil* wanamaanisha nini?
2/ Tunajuaje *Torah*, *Zabur* na *Injili* yenye Biblia ni ya asili na hayaja chafuliwa?
3/ Jinsi gani Uislamu ni mtego?
4/ Ni vipi Uislamu inazuia maendeleo?
5/ Swali lingine?

Sheria inasema mtu akitoka Uislamu anafaa: A. Afukuzwe
B. Aadhibiwe
C. Auawe

**/18/ Utetezi** Waislamu kwa Afrika Mashariki wanapenda kutengeneza mihadhara. Wahubiri wao hawahubiri Uislamu, ila wanaupinga Ukristo. Wengine wao wamefanya utafiti kwa Biblia na wanajaribu kudhihirisha udhaifu wote wa imani ya Ukristo, ili waweze kuwavuta watu kwa Uislamu. Inamhitaji Mkristo kuwa na msimamo dhabiti na ujuzi wa kutosha ili aweze kugundua uongo na udanganyifu wa Waislamu hawa. Hii inahitaji masomo zaidi, na ujuzi mzuri wa kibiblia.

Qur'an inaongea sana juu ya Yesu, anayeitwa na Waislamu kwa jina la 'Isa'. Ni vizuri kujua jinsi Qur'an inaongea juu ya Yesu. Qur'an inasisitiza kuzaliwa kwa Yesu kwa ajabu (Q. 3:47). Sura 3:59 inaonekana kusema Yesu aliumbwa (au inawezakuwa tu Adamu aliumbwa). Qur'an inasema Yesu alifanya miujiza mingi (Q. 5:110). Inasema pia Yesu alibarikiwa na Mungu, alitiwa nguvu kwa Roho Mtakatifu, hakukosea kwa ujumbe wake na mwenendo wake, ujumbe wake ulikuwa wa pekee, alijua yote, na ni mpatanishi aliye karibu na Mwenyezi Mungu. Qur'an inapinga Utatu (lakini inaamini Utatu unaoaminiwa na Wakristo ni wa Mungu, Yesu na Maria). (Q. 4:171 + Q. 5:116). Qur'an inapinga Yesu kuwa mwana wa Mungu (Q. 19:34+35, Q. 4:48), na anayesema Yesu ni Mungu anahesabiwa anafanya dhambi

mbaya ya *shirk*. Qur'an inasema wazi Yesu hakufa (Q. 4:156-158), kwa hivyo bado yuko hai, na atarudi. Lakini Waislamu wanasema akija atakuwa Mwislamu!

1/ Mihadhara ni nini? Umeshasikia ingine? Eleza.
2/ Kwa nini Qur'an inamwita Yesu kwa jina la Isa?
3/ Jadiliana juu ya mafundisho ya Qur'an juu ya Yesu.
4/ Eleza matokeo ya imani ya Waislamu kusema Yesu hajafa.
5/ Swali lingine?

Qur'an inafahamu Utatu wa Mungu kama
A. Baba, Mwana, Maria
B. Baba, Mwana, Roho
C. Baba, Mwana, Malaika

**/19/ Ukweli wa Mwungano wa Umungu na Uanadamu wa Kristo**

1/ Uthibitisho kutoka kwa wanabii: Isaya 9:6, Isaya 7:14, (Mt. 1:23), Zaburi 110:1, Miaka 5:2.
2/ Uthibitisho kwa maneno ya Yesu: Yo. 8:23, Yo. 17:5, Yo.8:23, Yo. 3:13, Ufunuo 22:13. Yesu yu mahali pote: Mt. 18:20, Mt. 28:19-20.
3/ Uthibitisho kwa majina yake na matendo ya Mungu: Yesu muumbaji Jo. 1:3+4, Kol.1:16, Waef 3:9. Uwezo wake kufufua; Lk. 7:12-15, Yo. 11:43-44. Atahukumu dunia: Mt. 25:31-32, Yo. 5:22. Anastahili kuabudiwa Yo. 5:23, Zab. 2:11 + 12. Husamehe dhambi Mk.2:5, Mk. 2:8-12. Hutoa uzima wa milele Yo.10:27-28. Yu sawa na Baba Yo. 14:8-11. Alikubali kuabudiwa Yo. 9:35-38.
4/ Uthibitisho kutoka wanafunzi: Yo. 20:28, 1 Yo. 5:20, Rumi 9:5.

1. Jadiliana juu ya Umungu wa Kristo.

Yesu alikuwa:
A. Mungu sio mtu
B. Mtu, sio Mungu
C. Mungu na pia mtu

**/20/ Umoja na Nafsi Tatu za Mungu** Katika Uungu: Baba (2 Thes. 2:16), Mwana (Waeb. 1:8), Roho (Matendo 5:3-5).
Katika Ubwana : Baba (Lk. 10:21), Mwana (Matendo 10:36), Roho (2 Cor.3:17).
" Umilele : Baba (Daniel 6:26), Mwana (Ufunuo 1:8) Roho (Waeb. 9:14).
" Uwezo kuwepo kila mahali: Baba (Waefeso 4:6), Mwana (Mt. 18:20), Roho (Zab.139:7-10).
Kustahili kuabudiwa: Baba (Yo. 4:23), Mwana (Wafil. 2:10-11), Roho (Warumi 8:26-28).
Tabia ya Ukweli: Baba (Yo. 17:17), Mwana (Yo. 14.6), Roho (Yo. 14:16-17).
Tabia ya Upendo: Baba (Yo. 16:27), Mwana (Yo. 15:14-15), Roho (2 Tim. 1:7).
Tabia ya Utakatifu: Baba (Yo. 17:11), Mwana (Lk. 1:35), Roho (Waef. 4:30).

1. Jadilian juu ya imani ya Utatu.

Nani anayeuwezo kuwepo kila mahali?
A. Baba, Roho na Mwana
B. Baba tu
C. Roho tu